GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **253** Muharram-Safar **1447** AH Julai– **2025** Wafaa **1404** HS BEI TSH 800/=

WAYAHUDI KUMHUKUMU YESU KRISTO ADHABU YA KIFO JE WALIKUWA SAHIHI??

Kwa mtazamo wao walikuwa sahihi; kwa sababu walitumia maandiko. Torati 13:1--9 na 21:22--23;

Kama walifuata na kutekeleza sheria; kwa nini walaumiwe na Mwenyezi Mungu?

Mathayo 23:37; Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!

Hakuna kitu kibaya sana Kwa mtu au mwanadamu yeyote kama kuwa na dhana mbaya, chuki, husuda na uongo. Mambo hayo yanamvuta mtu au mwanadamu yeyote kuelekea kwenye dhambi na makosa katika jamii.

UK. 04



Bishara Adhimu ya Kurani Tukufu

(Sheikh Shahab Ahmad, Mtwara)

Bishara mojawapo ya zama ya Masihi Aliyeahidiwa[as] iliyoelezwa ndani ya Kurani tukufu ni kwamba وَاِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ yaani sahifa zitakapoenezwa. Hii ni aya ya 11 ya sura at-Takwir sura ya 81. Katika aya hii mna bishara muhimu na adhimu ambayo ilitimia sawasawa kwa wakati wake.

Barua za Mahubiri

Awali ya yote bishara hii ilitimia katika maisha matakatifu ya Mtume Muhammad[SAW]. Aliamua na kupanga kuandika barua ya kuwahubiri wafalme wa nchi mbalimbali wakati ule. Baada ya tukio la Mkataba wa Hudaibia mnamo mwaka wa 6 Hijiria Mtume Muhammad[SAW] aliandika barua hizi kwa Kaisari mfalme wa Roma, Kisra mfalme wa Uajemi, Makukas mfalme wa Misri na Najashi mfalme wa Uhabeshi. Hivyo, maandiko matakatifu ya Mtume Muhammad[SAW] yalipelekwa katika nchi mbalimbali duniani.

Zama ya Kueneza Mwongozo

Katika maisha ya Mtume Muhammad[SAW] mwongozo ulikamilika yaani sheria ya Kurani Tukufu ilikamilika. Hakuna sheria nyingine yoyote itakayopatikana baada ya Kurani Tukufu.

Hata hivyo, zama ya kueneza mwongozo huu kufikia katika maeneo yote duniani ilitakiwa kuwa zama ya Masihi aliyeahidiwa[as]. Ndio maana Mwenyezi Mungu alihakikisha njia mbalimbali za kueneza dini ya Uislamu zipatikane katika zama ya Masihi aliyeahidiwa. Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyyah anasema:

«Kwa sababu zile njia na nyenzo bado hazikupatikana ambazo zilihitajika kwa ajili ya kuwaunganisha binadamu wote duniani, na zilizohitajika kurahisisha safari za bahari na za nchi kavu, na vifaa bado havikupatikana vilivyohitajika kutunga na kuchapisha vitabu vya kidini kwa wingi duniani, na binadamu bado hawakufahamu kuhusu lugha mbalimbali, na bado dini zote hazikuwa pamoja kwa ajili ya ulinganishi. ... hivyo, elimu ya Mwenyezi Mungu ilipanga zama nyingine kwa ajili ya kukamilisha uenezaji wa mwongozo, ambapo nyenzo zingepatikana kwa ukamilifu kwa ajili ya mahubiri.»
(Tohfa e Golarwia, Rohani Khazain, J. 18, UK. 258)

Kwa mujibu wa bishara za Kurani tukufu vifaa, nyenzo na njia zilizokamilika kwa ajili ya kueneza mwongozo zilipaswa kupatikana katika zama za Masihi Aliyeahidiwa. Jinsi ambavyo imeelezwa katika aya za mwanzo za Sura At-Takwir kwamba katika zama hizo usafiri wa namna mbalimbali utapatikana, watu watapata njia mbalimbali na vitabu vitachapishwa kwa wingi. Yaani dunia licha ya ukubwa wake itakuwa ndogo kwa sababu ya upatikanaji wa vifaa. Mtume Mtukufu[SAW] alieleza jambo hili katika Hadithi yake moja akisema يُقْبَضُ لَهُ الأَرضُ yaani ardhi itakunjwa au itasogezwa kwa ajili yake. (Kanzul Ummaal, kitabul Kiyama, Dhikru Yajuja Majuja)

Na hii ilikuwa ni zama ambapo ushindi wa Uislamu ulipangwa kama ilivyoahidiwa katika aya hii

هُوَ الَّذِیۡۤ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَہٗ بِالۡہُدٰی وَ دِیۡنِ الۡحَقِّ لِیُظۡہِرَہٗ عَلَی الدِّیۡنِ کُلِّہٖ

Tafsiri: Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili Aishindishe juu ya din izote. (Sura at-Tauba 9:33)

Kwa miaka mingi hakukuwa na miundombinu au mitambo ya kuchapisha vitabu kwa wingi. Vitabu viliandikwa kwa mkono na nakala kadhaa tu zilipatikana. Ndio maana kwa sababu ya muda mrefu kupita vitabu vilivyoandikwa viliendelea kuchakaa na hatimaye vitabu vingi vikawa nadra kupatikana.

Kwa sasa tunakuta majina ya baadhi ya vitabu yakitajwa ndani ya vitabu vingine lakini vitabu vyenyewe

KUISHI MAISHA YA UNYENYEKEVU NA UMASKINI

UK. 08

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KUSAMEHE KULIKO TUKUKA

Kusamehe ni khulka njema. Ni kutambua ubinadamu wako kuwa wewe hukukamilika na kuna siku nawe utalazimika kuomba msamaha na kusamehe. Hiyo ni aina moja ya kusamehe.


Lakini khulka ya kumsamehe mtu wakati una nguvu na uwezo wa kumuadhibu, hicho ndicho kiwango cha hali ya juu cha kusamehe. Kiwango hiki kilichokamilika na chenye shani na utukufu mkubwa kilioneshwa na Mtukufu Mtume Muhammadsaw. Ni kweli ya kwamba Mtume Muhammadsaw alikuwa na khulka njema na ametumwa kuwa rehema kwa dunia nzima.

Mtukufu Mtume Muhammadsaw alikuwa ametoka vitani ilikuwa ni wakati wa mchana na jua lilikua kali, masahaba walitafuta kivuli na Mtukufu Mtume Muhammadsaw akapata kivuli mbali kidogo kutoka kwa Masahaba zake. Usingizi ulimpitia na ghafla adui mmoja kwa jina la Dathur alikwenda taratibu na kuchukukua jambia ya Mtukufu Mtume Muhammadsaw iliyokuwa juu ya Mti. Yule adui alichukua jambia lake na kusimama mbele yake huku akisema, ewe Muhammad nani anaweza kukuokoa kwa hivi sasa? Kwa sauti iliyo imara isiyokuwa na wasiwasi wowote Mtukufu Mtumesaw alimjibu ALLAH, sauti ile yenye uhakika na nguvu kubwa ilipotoka yule adui akaanza kutetemeka mwili mzima. Katika hali hiyo ya kutetemeka jambia lile likadondoka chini na Mtukufu Mtumesaw akaliokota na kumuuliza yule adui nani anaweza kukuokoa kwa hili? huku akitetemeka aliomba msamaha na Mtukufu Mtumesaw akamsamehe na kumuacha aende zake. Na huyo ni adui aliyetaka kutoa maisha yake.

Siku ya ushindi wa Makka haina mfano katika historia ya binadamu. Kwa miaka 13 nyuma Mtukufu Mtumesaw na masahaba zake walikuwa wameteswa. Waislamu wakawekewa vikwazo vya kutopata chakula baadhi ya masahaba wakahamia Abysinia na Mtukufu Mtumesaw ikabidi kufanya Hijra ya kwenda Madina na hata huko Madina, Makureish wakaendeleza uhasama, njama na vita. Sasa waislamu walikuwa wameshinda vita na ishara tu kutoka kwa Mtukufu Mtumesaw ya kuwaua ingetekelezwa kwa haraka. Lakini hakufanya hivyo bali kwa sauti ya upole iliyojaa huruma aliwauliza, niambie niwatendee nini? Wakionyesha unyenyekevu, aibu na huku wameinamisha vichwa chini walijibu tunatarajia kutoka kwako yale Nabii Yusuphas aliyowatendea ndugu zake. Mtukufu Mtumesaw aliposikia kauli hiyo bila kujali mateso ya nyuma alisema "Nendeni hakuna lawama kwenu Allah Awasamehe kwa hakika yeye ni msamehevu. Nendeni nyote mko huru kwenda.

Kwa matukio haya mawili tunapata Dawa mujarabati ya matatizo tuliyonayo Duniani kwa hivi sasa. Hakuna kosa unaloweza kutendewa na ukakosa kusamehe. Wapo waliofaidika na kujifunza kutoka katika maisha ya Mtukufu mtume Mtukufu Mtumesaw. Samora Machel, Raisi wa kwanza wa Msumbiji alipigana vita vya msituni na Wareno na vibaraka wao wana Msumbiji. Yalikuwa mauaji makubwa na ukatili, Samora Machel aliwasamehe wote Nchi hiyo ilipojipatia uhuru. Nelson Madiba Mandela miaka 27 alikuwa kwenye kisiwa cha Robben pamoja na Makomredi wenzie. Huku nyuma serikali ya makaburu iliendelea kuwatesa wananchi kupitia sera yao ya ubaguzi wa rangi, mauaji makubwa ya Sharperville na mauaji ya Soweto. Yote haya yalikuwa maumivu makubwa, hata hivyo Nelson Madiba Mandela alitoka jela ukafanyika uchaguzi na akachaguliwa kuwa Rais wa kwanza aliyechaguliwa kidemokrasia na wananchi wa Afrika Kusini siku ya uhuru alitamka yaliyopita si ndwele, tugange yajayo.

Jomo Kenyatta aliyemuomba Sheikh Mubarak Ahmad KITABU cha Maisha ya Muhammad (saw), alipotoka gerezani aliwasamehe wazungu waliomuweka ndani na kumbebesha msalaba wa vita vya Maumau. Alimwahidi Sheikh Mubarak Ahmad ukipatikana uhuru atawasamehe wote. Na kweli alitimiza ahadi yake. Kuinusuru Dunia tuna wajibu wa kusambaza mafundisho aliyoyaleta na kuyaonesha kwa vitendo Mtume Muhammadsaw. Mafundisho mazuri bila vitendo ni mithili ya jangwa na hakuna kitakachomea.




QUR'AN TUKUFU

Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa hapo kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri.

Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

هُوَ الَّذِیۡ بَعَثَ فِی الۡاُمِّیّٖنَ رَسُوۡلًا مِّنۡهُمۡ یَتۡلُوۡا عَلَیۡهِمۡ اٰیٰتِهٖ وَ یُزَکِّیۡهِمۡ وَ یُعَلِّمُهُمُ الۡکِتٰبَ وَ الۡحِکۡمَةَ ٭ وَ اِنۡ کَانُوۡا مِنۡ قَبۡلُ لَفِیۡ ضَلٰلٍ مُّبِیۡنٍ ۙ﴿۳﴾

وَّ اٰخَرِیۡنَ مِنۡهُمۡ لَمَّا یَلۡحَقُوۡا بِهِمۡ ؕ وَ هُوَ الۡعَزِیۡزُ الۡحَکِیۡمُ ﴿۴﴾



NUKUU YA HADITHI

Ilisimuliwa na Hazrat Abu Hurairah (ra) ya kwamba Mjumbe wa Allah (saw) alisema: Mtakuwaje atakaposhuka Ibn Mariamu kati yenu naye atakuwa Imamu kutoka miongoni mwenu.

عن ابی هریرة رضی الله عنہ قال: قالَ رسولُ اللهِ صلّی اللهُ علیہ وَسلّم: کیف أنتم إذا نَزَل ابْنُ مریمَ فِیکُم وَإمَامُکُمْ مِنْکُمْ
بخاری کتاب الانبیاء باب نزول عیسیٰ بن (مریم



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Ikumbukwe kuwa katika neno Imamu wa zama, wanaingia Nabii, Rasuli, Muhaddathi na Mujaddidi kwa jumla; lakini watu ambao hawajaamrishwa kuwaongoza viumbe wa Mungu wala hawajajaliwa sifa hizo kamilifu, watu hao hata wakiwa mawalii au watawa sana hawawezi kuitwa ni Imamu wa zama.

Sasa mwishoni swali hili linabakia kuwa katika zama hizi Imam wa zama ni nani ambaye Waislamu wa kawaida na watawa na waotaji njozi na wapokeaji wamelazimishwa wa na funuo wote hao Mwenyezi Mungu kumfuata? Basi nasema wakati huu bila hofu yoyote kuwa kwa fadhili na hisani za Mwenyezi Mungu mimi ndimi Imamu wa zama na ndani yangu Mwenyezi Mungu Amejumuisha alama na masharti yote hayo na Amenituma mwanzoni mwa karne hii ambamo miaka kumi na mitano tayari imeshapita. Na nimedhihiri katika wakati ambapo itikadi za Waislamu zilijaa hitilafu, na hakuna itikadi isiyokuwa na hitilafu. Kadhalika fikara isiyokuwa sawa kabisa kuhusu kushuka kwa Masihi ilikuwa imeenea; na katika itikadi hii pia hali ya hitilafu ilikuwa kwamba baadhi yao waliamini Hadhrat Isaas yuko hai, na wengine waliamini amekwisha fariki; baadhi yao waliamini kwamba atashuka kimwili na wengine walikuwa na itikadi atashuka mtu mwingine kama mfano wake. Baadhi yao wakaamini atashuka Dimashki na wengine katika Makka, wengine katika Baitul Muqaddas na wengine ndani ya Jeshi la Kiislamu, na wengine walidhania kuwa atashuka katika India. Basi, rai hizo na kauli hizo zote zilizotofautiana zilimhitaji mwamuzi wa kutoa hukumu. Basi, Mwamuzi huyo ni mimi. (Haja ya Imamu, kur. 43,44)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Bishara Adhimu ya Kurani Tukufu

Kutoka uk. 01

havipatikani. Hapo tuwaone kudra maalum ya Mwenyezi Mungu na bishara adhimu ya Kurani tukufu ilivyotimia. Mitambo ya uchapishaji na matbaa zilianza kupatikana kabla ya ujio wa Masihi aliyeahidiwa[as].

Mageuzi makubwa katika sekta ya uchapishaji yaliletwa katika miaka ya 1450. Johannes Gutenberg alianzisha kiwanda cha uchapishaji. Kwa mujibu wa wanahistoria kabla ya kiwanda hiki vitabu 30,000 tu vilipatikana katika nchi zote za Ulaya. Idadi hii iliongezeka na kufikia zaidi ya vitabu milioni moja na laki mbili ndani ya miaka 50. Lengo halisi la kupatikana kwa vifaa hivi vya kisasa ni kueneza elimu ya kidini kuhusu Kurani Tukufu na mafundisho mengine ya Uislamu kupitia maandiko ya Seyyidna Ahmad[as]. Akieleza kuhusu aya ya وَاِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ katika kitabu chake "Aina Kamalaat e Islam" Hazrat Masihi aliyeahidiwa[as] alisema kuhusu vifaa hivi vya uchapishaji vilivyoanzishwa na wafuasi wa dini mbalimbali kwamba "hii nii kazi ya Mwenyezi Mungu, ambayo kwayo Anisaidie katika majukumu yangu na Aeneze mafundisho yangu, vitabu vyangu na nukta zangu za maarifa katika watu wote ili wazitegee masikio na kuongoka".

Hazrat Masihi aliyeahidiwa[as] katika kitabu chake "Hakikatul Wahyi" alitaja ishara ya uzinduzi wa matbaa na viwanda vingi vya uchapishaji na vitabu vingi kupigwa chapa kuwa ni ishara namba 6 ya ukweli wake. Pia alisema: "Jambo la msingi ni kwamba zama ambapo Nabii yeyote wa Allah hutumwa duniani basi mambo yote makuu na mageuzi yote yanayopatikana katika zama hizi hunasibishwa kwake."
Hivyo, kwa mujibu wa aya hiyo, kuanzishwa kwa viwanda vya uchapishaji ni hoja adhimu ya ukweli wa Masihi aliyeahidiwa[as]. Yeye mwenyewe akieleza bishara mbalimbali zilizomo katika Sura at-Takwir anasema:
"وَاِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ yaani zama za mwisho ni ile ambapo vitabu na machapisho vitachapishwa kwa wingi kiasi kwamba havijawahi kuchapishwa hivyo huko nyuma. Hii inaashiria vifaa ambavyo kwavyo vitabu huchapishwa siku hizi na kisha hupelekwa umbali wa kilomita nyingi kwa kupitia treni au garimoshi."
(Chashma-e-Maarifat, Ruhani Khazain, Juz. 22, uk. 322).

Kisha safari nyingine akieleza bishara hii akasema:
"Mwenyezi Mungu hakueleza ishara moja tu kuhusu zama hizi za mwisho ambapo watu wote watakusanyika kwa dini moja, bali ishara nyingine nyingi zimeelezwa ndani ya Kurani Tukufu, katika hizo mojawapo ni kwamba... njia zitapatikana zitakazofanya vitabu viongezeke. (Hii inaashiria mitambo ya uchapishaji)... ishara hizi zote zimetimia katika zama hizi. Mwenye akili ana kila sababu ya kuelewa kuwa Mwenyezi Mungu Alinituma katika zama ambapo ishara zote za ujio wangu zilizoandikwa ndani ya Kurani Tukufu zimetimia."
(Lecture Lahore, Hotuba ya Lahore, uk. 48)

Baadhi ya wanazuoni, wafasiri na watoa maelezo walichukulia bishara hii kuwa itatimia siku ya Kiyama ambayo itakuwa siku ya mwisho. Na sahifa hizo ni orodha ya vitendo itayopatikana siku hiyo. Hapo swali linaibuka kwamba je, aya hii inahusikana na siku ya Kiyama tu au mambo ya hapa hapa duniani yameelezwa humo?
Seyyidna Ahmad[as] Masihi na Mahdi aliyeadhiwa ambaye alitumwa akiwa *Hakaman ad-lan* (hakimu mwadilifu) aliwahi kueleza kuwa bishara hizi zote zilizomo ndani ya Sura at-Takwir ni alama za zama ya Masihi aliyeahidiwa na hazihusiani na Siku ya Kiyama. Ndiyo maana anasema akieleza kuhusu aya ya 5 ya sura hii وَاِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ yaani, ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa:
"Wale ambao wanadhani kuwa aya hizi zinahusu Siku ya Kiyama hawafikirii kuwa ngamia watakuwaje na mimba katika Kiyama, kwani عشار (ishaar) yamaanisha ngamia wenye mimba. Kisha imeandikwa kuwa katika zama hizi Bahari zitaongezeka sana na kuenea kila upande na vitabu vitachapishwa kwa wingi. Hivyo, bishara hizi zote zilihusu zama hizi."
Halafu akasema:
"Kama bishara zisipotimia katika dunia hii, zitakuwaje na faida na kwa njia gani imani itaongezeka? Watu wasiojua huwa wanapachika kila bishara kuwa itatimia Siku ya Kiyama, na ukiwauliza husema kwamba ndani ya Kurani Tukufu hakuna bishara yoyote kuhusu dunia hii."
Mwana aliyeahidiwa Hazrat Khalifatul Masihi wa Pili[ra] alitoa maana tatu za neno نشر. 1. kueneza, 2. kufungua na 3. kumfufua mfu. Hivyo, kwa kuzingatia maana hizi alieleza maana tatu za bishara. Yaani bishara hii ilitimia kwa namna tatu ambazo ni kama hivi ifuatavyo.

1. Viwanda vingi vya uchapishaji wa vitabu, magazeti na machapisho vimeanzishwa duniani na njia nyingi zimeundwa za usafirishaji wa machapisho hayo kama treni au garimoshi n.k.

2. Kawaida ya kusoma vitabu imeongezeka kwa mfano katika maktaba ambapo watu hufika kusoma vitabu na wengine huazima vitabu na kuvipitia nyumbani. Kwa hiyo, inaonekana vitabu vimefunguliwa badala ya kuendelea kufungwa.

3. Namna nyingine ya kutimia kwa bishara hii ni kwamba wataalamu wa akiolojia walitafsiri vitabu vilivyoandikwa katika lugha za zamani sana. Kwa njia hii tafsiri hizi zimefufua vile vitabu. Kwa mfano, wataalamu waligundua hieroglifu yaani maandiko ya Wamisri wa kale (hieroglyphics) na wakafufua maandiko hayo kwa kutoa maana na tafsiri yake.
(Imetolewa katika Tafsir-e-Kabir, juz. 8, kur. 225-224)

Mbali na hayo, sawa na maendeleo ya teknolojia katika zama hizi bishara hii inaendelea kutimia kila kukicha. Kwa njia ya mtandao wa intaneti vitabu na elimu ya kila aina imeenezwa duniani. Tovuti na kurasa mbalimbali zimepata sura ya machapisho na sahifa mitandaoni. Na hizi zote zinathibitisha ukweli wa bishara ya Kurani Tukufu iliyotakiwa kutimia katika zama ya Masihi aliyeahidiwa.

Ahmadiyya itumiavyo machapisho
Kuanzia mwanzo Jumuiya ya Ahmadiyya iko mstari wa mbele katika kutumia machapisho kwa ajili ya mahubiri. Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu leo hii pia inaendelea kutoa mafunzo ya dini kupitia vitabu, magazeti na machapisho.

Mwanzilishi wa Jumuiya, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi na Mahdi aliyeadiwa[as] kwa kumfuata Bwana wake Mtume Mtukufu Muhammad[SAW] aliandika barua za mahubiri kwa wafalme na viongozi wa zama zake. Pia, alichapisha maelfu ya vitabu, vipeperushi na matangazo kueleza mafundisho yake katika nchi mbalimbali. Machapisho hayo yalikuwa katika lugha mbalimbali na hata katika maisha yake tayari yalifika hadi Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Yunani, Urusi, Marekani na kadhalika.

Kisha Masihi aliyeahidiwa[as] alianzisha jarida la Kiingereza liitwalo Review of Religions. Matoleo yake yalikuwa yanapelekwa katika nchi za Marekani na Ulaya. Mahubiri ya ajabu yalianzishwa kwa njia hii na dunia ikashuhudia kutimia kwa bishara ya jua litachomoza upande wa Magharibi. Vitabu na machapisho haya ya mwanzo kabisa yalipelekwa na Masihi aliyeahidiwa[as] mwenyewe.

Leo, kupitia Ukhalifa wa Masihi aliyeahidiwa[as] vitabu, majarida, magazeti na maandiko ya kidini yanaendelea kuchapishwa na kuenezwa duniani. Mpaka sasa, Kurani Tukufu imeshatafsiriwa katika lugha zaidi ya 70 duniani. Mpango unaendelea wa kutafsiri vitabu vya Hadithi za Mtume Muhammad[SAW] na kusambaza mafundisho ya dini ya Uislamu duniani. "Ruhani Khazain" (Hazina za Kiroho) yaani vitabu na maandiko ya Seyyidna Ahmad[as] zinatafsiriwa katika lugha mbalimbali duniani na kusambazwa ili watu wapate kuelimika. Viwanda vya uchapishaji na matbaa zimekuwa chanzo kikuu cha kutimia kwa bishara hii. Vilevile, intaneti, simu janja na mitandao ya kijamii vifaa hivi vyote vinasaidia katika kufikisha maandiko na machapisho kwa watu wengi sana. Ndani ya sekunde kadhaa machapisho ya kidini yanaweza kumfikia mtu anayekaa sehemu yoyote duniani. SubhanAllah, ni ajabu iliyoje ya kutimia kwa bishara ya Kurani Tukufu na kudhihirisha kwa ukweli wa Uislamu na Mtume Mtukufu[SAW].

MAPENZI YA MUNGU
Gazeti la Mapenzi ya Mungu nalo ni ushuhuda tosha wa kutimia kwa bishara hii adhimu. Mwaka 1936, gazeti hili lilianza kuchapishwa, kutoa mafunzo na kuelimisha jamii kuhusu mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam na lingali linaendelea kutimiza wajibu wake.

Safari yake hii imejaa ufafanuzi wa mafundisho ya Kurani Tukufu, Hadithi, maisha ya Mtume Muhammad[saw] na masahaba, kauli za Masihi aliyeahidiwa[as] na Makhalifa zake, mashairi na matukio mbalimbali yanayosisimua imani ya wanajumuiya wengi. Watu wengi walinufaika na makala zake. Wengi walijiunga na Jumuiya ya Masihi aliyeahidiwa na Imam Mahdi kupitia mahubiri yake. Wanajumuiya wengi nchini Tanzania wanalisubiri na wanapenda kujipatia nakala yake kila mwezi. Wengine walioko ughaibuni wanalipitia kwa njia ya mtandao.

Gazeti hili linaendelea kuwa msemaji wa Khalifatul Masihi kwa wasomaji wa lugha ya Kiswahili. Waandishi huwa wanachangia kuandika makala nzuri na hivyo wanaonesha upendo wao na gazeti hili. Mwenyezi Mungu Awabariki wote na Alipatie gazeti hili maendeleo makubwa na wasomaji wake wapate nuru na baraka za Ukhalifa kupitia gazeti hili. Aamin.

WAYAHUDI KUMHUKUMU YESU KRISTO ADHABU YA KIFO

Kutoka Uk wa 1..

Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuyaelewa maandiko ya vitabu vya Mwenyezi Mungu kwa sababu kutokuelewa kwa neno au jambo ni chanzo kikubwa cha mambo hayo yaliyotajwa hapo juu.

Katika Vitabu vya dini Mwenyezi Mungu na manabii wake wanaongea kwa mifano, methali, misamiati na matabiri. Mwanadamu anapokuwa katika jambo lake anakuwa mgumu kupokea na kuelewa jambo jingine jipya na la ghafla. Hali hii ndiyo iliyowapelekea Mayahudi kutokumuelewa Yesu kwa maoni yao na wakamhukumu kifo.

YESU AJITANGAZA KWA MAYAHUDI NAO WALISHINDWA KUMUELEWA

YESU alikuwa anaongea kwa mifano, mithali, misamiati na matabiri alijiita mwana kondoo na akajitangaza kwa Mayahudi kwamba yeye ametumwa kwao kama nabii na mtu akifuata mafundisho yake hataona mauti milele. Mt. 15:24; 13:34--35 na Yoh 8:51--52; 10:1--11;

Yohana 6:41-42; Basi Wayahudi wakamnung'unikia, kwa sababu alisema, Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni.

Wakasema, Je! Huyu siye Yesu, mwana wa Yusufu, ambaye twamjua babaye na twamjua mamaye? Sasa asemaje huyu, Nimeshuka kutoka mbinguni?
Je ni kweli YESU KRISTO AMESHUKA KUTOKA MBINGUNI?

Yohana 10:4,6; Naye awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia; na wale kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake. Mithali hiyo Yesu aliwaambia, lakini wao hawakumuelewa na mambo hayo aliyowaambia. nk....

Yesu alionekana ni muongo kwa kuwaambia mayahudi hakuna mtu aliyepaa kwenda MBINGUNI.Yoh 3:10--13;

Mayahudi Walitoa ushahidi wa maandiko kuhusu Kupaa kwa Enoko na Eliya;, 2Wafal 2:11;

Yesu alionekana muongo mkubwa alipowaambia mayahudi habari ya Yohana mbatizaji ndiye Eliya. Mt 17:10--13;

Mayahudi walithibitisha kwa maandiko ni Mwenyezi Mungu mwenyewe Aliahidi kumrejesha Eliya hasa kwa mara ya pili MALAKI 4:1--6;

Yohana 10:33; Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya utumwa. kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u mungu. Kwa kuto kumuelewa mifano na misemo yake ndipo wakadhani huyu amekufuru. Wakamuongezea mambo ya uchochezi upande wa serikali kwa makosa ya uhaini, kwa kujiita mfalme wa mayahudi na anazuia ulipaji wa kodi za serikali nk. Anastahili kuhukumiwa ADHABU ya KIFO.

Watu wa dini waliishinikiza serikali ili imuhukumu adhabu ya kifo. Kwa mujibu wa mafundisho na maandiko ya torati mtu au mwanadamu kujiita mungu ni makufuru makubwa sana.
Hukumu yake ni kupigwa kwa mawe na kuwambwa msalabani mpaka mtu huyo afe na mzoga wake usilale pale. Uzikwe siku hiyo hiyo.

Kumbukumbu la Torati 13:6,10; Atakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mamaako, au mwana wako, au binti yako, au mke wa kifuani mwako, au rafiki yako aliye kama moyo wako. Akikuambia, twende tukaabudu miungu mingine usiyoijua wewe wala baba zako; nawe mtupie mawe hata afe; kwa kuwa alitaka kukupotoa na bwana, Mungu wako aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya Kumbukumbu la Torati 21:22-23: Akiwa mtu ametenda dhambi ipasayo kufa, akauawa, nawe ukamtundika juu ya mti; mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku iyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu; usije ukatia unajisi katika nchi yako akupayo bwana, Mungu wako, iwe urithi wako. JE WALIKUWA SAHIHI ?

Ewe mdau isitumike wala usitumie vitabu vya Mwenyezi Mungu kuukataa ukweli kama mayahudi.


Ewe mkristo na baadhi ya waislamu; jua lengo la Mwenyezi Mungu.Ufikie malengo yaliyokusudiwa; tafadhali tafakari chukua hatua stahiki; bado muda unao !!!!!

Mayahudi walitumia maandiko ya Mwenyezi Mungu kuukana ukweli tu hiyo ni njia mbaya sana isifuatwe.

Huo ndio mti wa matunda ya mizabibu uliolaaniwa na Mwenyezi Mungu.!!

Isaya 5:1--7:- mwenye masikio na asikie

neno letu la mwisho ni
UPENDO KWA WOTE; BILA CHUKI KWA YEYOTE



MAJIBU YA BAADHI ZA SHUTUMA/PINGAMIZI DHIDI YA SEYYIDNA AHMAD[AS] KUWA KWAKE IBN MARYAM

بسم الله الرحمٰن الرحيم

Swali na Jibu la Hazrat Ahmad a.s:
Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s ameandika mara nyingi kwamba kumwita kafiri mtu anayesoma kalima au anaye elekea kibla si sahihi. Hii inaonyesha wazi kwamba, mbali na wale wanaomkana na hivyo kuwa makafiri, kumkataa yeye pekee hakumfanyi mtu kuwa kafiri. Hata hivyo, ulimwandikia Abdul Hakim Khan ukisema kwamba yeyote ambaye amesikia ujumbe wako na hajakukubali si Muislamu. Kauli hii inaonekana kupingana na maandiko yako ya awali, kama vile {Tiryakul Qulub}, ambapo ulisema kuwa kukukataa hakumfanyi mtu kuwa kafiri.
Sasa unasema kwamba kukukataa wewe kunamfanya mtu kuwa kafiri.

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad alijibu a.s :

"Ni ajabu kwamba unafanya tofauti kati ya mtu anayeniita kafiri na mtu anayenikataa, na kuwatofautisha kuwa aina mbili za watu, ilhali mbele ya Mungu ni aina moja tu. Kwa sababu mtu anayenikataa hufanya hivyo kwa sababu ananiita mwongo. Lakini Mungu anasema kwamba anayemzulia Mungu ni kafiri mkubwa zaidi, kama alivyosema, ndani ya kurani tukufu kuwa

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ

Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anaye mtungia uongo Allah au anazikadhibisha ishara zake. 7:38

''Kwa hivyo, mbele ya mtu anayenikana, mimi ni mtu niliyezua uwongo dhidi ya Mungu. Katika hali hii, siyo tu kwamba mimi ni kafiri, bali mimi ni kafiri mkubwa zaidi. Lakini ikiwa mimi si mwongo, basi kwa hakika ukafiri huo utamwangukia yeye, kama Mwenyezi Mungu Mwenyewe alivyoeleza katika aya hii. Aidha, mtu anayenikataa pia anamkana Mungu na Mtume Wake kwa sababu kuna unabii kuhusu mimi kutoka kwa Mungu na Mtume (saw). Mtume (SAW) alitabiri kwamba, Masihi aliyeahidiwa atatokea kutoka miongoni mwa umma wake, na alisema pia kwamba alimwona Masihi, mwana wa Mariamu, miongoni mwa manabii waliofariki katika safari yake ya Mi'raj."

Hazrat Ahmad a.d anaendelea kueleza kwamba kumkataa yeye kunamaanisha kumkataa Mungu, ukweli wa Mungu, na unabii wa Mtume Muhammad (saw). Kwa hivyo, mtu kama huyo hawezi kuchukuliwa kuwa muumin wa kweli.

Hitimisho, Hazrat Mirza Ghulam a.s Ahmad hakuwahi kuanzisha tangazo la ukafiri. Badala yake, ni wapinzani wake walioanza kumtangaza kuwa kafiri, na kulingana na hadithi ya Mtume (saw), hukumu ya ukafiri inarudi kwao wenyewe. Hazrat Ahmad a.s na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya wanazingatia tu mafundisho ya Quran na Mtume (SAW) kuhusu suala hili.

Ufafanuzi zaidi wa suala hili ulitolewa na Hazrat Masih Maud (a.s.) akisema:
"Hatuwatoi nje ya Uislamu wale wanaokiri Kalima mpaka watakapotuita makafiri na kwa kufanya hivyo wao wenyewe wawe makafiri. Wale ambao hawatuiti makafiri, hatuwaiti makafiri kamwe, lakini wale wanaotuita makafiri, kama hatutawaona makafiri, basi tutakuwa tunapinga Hadith, na ni suala lililokubaliwa na wote, na hilo haliwezekani kwetu."(Malfoozat, Juzuu ya 10, uk. 376-377)

KuKuwaita wapinzani wake kafiri kulifanywa na wapinzani wa Hazrat Masih Maud (a.s.), na kwa sababu hiyo wao wenyewe walihusika na hilo na kwa mujibu wa uamuzi wa Hadith ya Mtume (s.a.w.) wakawa makafiri. Hazrat Masih Maud (a.s.) hakumuita yeyote kafiri.

Msimamo wa Hazrat Masih Maud (a.s.) na Jamaat ya Ahmadiyya ni wazi na unakubaliana na sheria. Hazrat Masih Maud (a.s.) hakumuita yeyote kafiri, bali Mtume Muhammad (s.a.w.) alisema kuwa yule anayemuita Mwislamu mwingine kafiri, yeye mwenyewe anakuwa kafiri. Kwa hiyo, hapa tena mtoa hoja amewapotosha watu kwa makusudi.

Kuhusu kumkataa Masihi na Mahdi. Ukweli ni kwamba Hazrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani (a.s.) ndiye Masihi wa Ahadi na Mahdi aliyetarajiwa, ambaye alitumwa na Allah kwa mujibu wa maandiko ya zamani na utabiri wa Mtume Muhammad s.a.w. Kwa hiyo, kumkataa yeye ni sawa na kumuasi Allah na kukataa mafunzo ya Mtume (s.a.w.). Mtume Muhammad s.a.w. alisema kuhusu Masihi na Mahdi wake:

"اِذَارَاَيْتُمُوْهُ فَبَايِعُوهُ"

"Unapomwona, basi ingia katika bai'at yake."
(Ibn Majah, kitabul fitan, Sura ya Kuja kwa Mahdi)
Swali hapa si kuhusu Hazrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani a.s. kama mtu binafsi, bali ni kuhusu nafasi ya Masihi na Mahdi, ambayo yeye aliwekwa na Allah. Kumuamini Masihi na Mahdi na kuingia katika bai'at yake ni amri ya Mtume Muhammad s.a.w. na pia alisema:

"مَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِيْ عُنُقِہٖ بَيْعَةٌ مَاتَ مِيْتَةً الْجَاهِلِيَةِ"

"Yeyote atakayekufa bila kuwa na bai'at shingoni mwake, atakufa kifo cha kijahiliya." (Muslim)
Baada ya jibu hili kamili, haya ni baadhi ya mambo ambayo wasomaji wataona ya kuvutia. Kwa mfano, imeandikwa: Mtume Muhammad (s.a.w.) alisema,"Yeyote anayekanusha kuja kwa Mahdi, amekanusha kile kilichoteremshwa kwa Muhammad."

(Yanabi' al-Mawaddah, Sura ya 78, na Alama Sheikh Suleiman bin Sheikh Ibrahim, aliyekufa 1294 AH)

Tafsiri: Mtume Muhammad (s.a.w.) alisema, "Yeyote atakayekanusha kuja kwa Mahdi, amekanusha yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad."

Vivyo hivyo, wanazuoni maarufu wa Ahlul-Hadith wameandika fatwa:

" مَنْ كَذَّبَ بِالْمَهْدِيِّ فَقَدْ كَفَرَ"

"Yeyote anayemkanusha Mahdi, hakika amekufuru."

(Hujjajul-Karama, uk. 351, na Nawab Siddiq Hassan Khan Bhopali, Matbaa Shahjahan Press Bhopal)
Kwamba yeyote anayemkataa Mahdi amekufuru.

Nawab Noorul Hasan Khan wa Bhopal aliandika: "Mtu yeyote... anayemkataa Mahdi, atakuwa kafiri." (Iqtirab al-Sa'a, uk. 100, mwandishi Nawab Noorul Hasan Khan)
Fatwa hizi si za Jamaat ya Ahmadiyya bali ni za wazee wa upande wa mtoa hoja na wenzake, na zinawasilishwa hapa kama hoja kwa ajili yao. Jamaat ya Ahmadiyya inasimama kwenye imani zinazotokana na aya za wazi za Qur'ani na Hadith zilizobainishwa wazi na Hazrat Masih Maud (a.s.) na kuzifanya kuwa msingi wa msimamo wao.

Bustani ya Washairi

WATAFUTA

Wewe watafuta jua, kutumia kibatali
Bileshi wajisumbua, kufunga hiyo safari
Maji ya mto najua, siyo sawa ya bahari
Mwana watupa kicheko, ukae na kufikiri.

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba Kiwalani - Dar es salaam.

Ukhalifa

Bisimilahi manani, Kwa upole nasimama
Machache Nayo moyoni,Kwa siku hii adhima
Kuwakumbusha nsani, ubora wa isilama
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Ulianzia zamani, Toka zile za adama
Lake lengo lipishani, hadi Leo tangu zama
Kuihimarisha dini, shirikini kutozama
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Khatamu nabiiyini, mara mbili lyahidiwa
Abubakari mwanzoni, umari akafatiwa
Baadaye othumani, naalii akapewa
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Radhi zamola manani, kwao tunawaombeya
Hivi mwakumbuka nini, baadaye lifwatiya
Ilivirugika dini, uchamungu kapoteya
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Huruma warahamani, Masihi katuleteya
Aje irudisha dini, yamuhamadi sawiya
Katutoa gerezani, Baraka zinatujiya
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Lipongiya mautini, khalifa lichaguliwa
Maulana nurudini, ndiye alochaguliwa
Kaisimamia dini, vurugu kuiondowa
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Wapili bashirudini, mwana aloahidiwa
Akaishindisha dini, kama livyotarajiwa
Amadiya duniani, kote wakaitambuwa
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Baada bashirudini, Nasiri alifwatiya
Akuacha wapinzani, jamati kuichezeya
Maulamaa wadini, chuki zikawazidiya
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Tahiri mwanachuoni, nafasi akashikiya
Katoka Pakisitani, landani akafikiya
Isilamu uzunguni, ikapata kueneya
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Masururi khamsani, Sasa tunamfatiya
Asifika Kwa Amani, Dunia kuitakiya
Mchamungu mwenyeshani, fahari ya jumuiya
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Walyopo isilamuni, wajibu kukumbushiwa
Ili uwende peponi, ukhalifa watakiwa
Niamuri ya manani, utii unapasiwa
Ukhalifa ni Baraka, kijitenga umotoni

Mtunzi
Masihi omary Stambuli kisagwa

1. ELIMU

Jifunze ilmu utavuna, maarifa na hekima aali
Elmu ina utukufu na dhima, hurahisisha kilicho ghali
Gumu likawa layina, utaheshimiwa watu watakujali

Kila mmuujiza uliofichikana, utatambua yake siri
Japo ndoto za mchana, utafahamu yake taa'wili
Akili yako itazindukana, magumu yakawa sahili

Zito likawa jepesi, wapata nguvu ya kusubiri
Mambo huwa mepesi, ukaweza mbali kusafiri
Ekaepukana na mikosi, yenye kudhoofisha mwili

Vitabu visome sana, mazito waweza badili
Akili yataka kusana, ndipo mengi utafidi
Utashirikiana na waungwana, wenye heshima na asili

Hofu yako itazama, nafsi yako itanawiri
Mola umkumbuke sana, usimuondoe katika akili
Ya leo sio ya jana, jifunze ilmu thaqili

Utaishi kwa mapana, utaondosha wako mushkili
Soma usiku na mchana, Mola atakujalia taufiki
Soma uzeeni na ujana, ujinga una madhili

Hakika ilmu itakulinda, na yako rasilimali
Utaepukana na inda, hutakuwa na dosari
Mola atakupenda, atakuondoshea kila hatari

Elmu nuru ing'aayo sana, huondosha giza likahama
Elmu chombo cha maana, usiwache nayo kushikamana
Japo umbali wa china, kaitafute siogope gharama

Elmu mbili zijue sana, ya dini na kimwili
Ala kuli hali, soma usifanye ubahili
Itakuondokea idhilali, moyo wako utanawiri

Soma kwa bidii, kila jambo kustahimili
Uvivu utupe mbali, utakuwa mtu kamili
Hakika ilmu ni mali, mali yataka tadbiri

Elimu ni nuru, kisha yataka maadili
Ikae katika suduru, Kisha yaongeza akili
Mola umshukuru, usome dua kwa takariri

Elmu ni bahari, weka mpango kamili
Mola Qahari, nia yako usibadili
Usifanye ufahari, usishike hili na hili

Weka mpango kamili, elimu uikabili
Elimu ni bahari, japo ile ya upili
Uwe mtu mahiri, usisahau jambo hili

Elimu huua ujinga, ikampandisha mja dhalili
Kisha hua kinga, humtoa mtu ujahili
Wendapo utaringa, soma upate nawiri

Utakapo utukufu na heshima, soma ilmu ikikubali
Ukweli na ubora wa kusema, na vitendo vyenye adili
Ukitaka umaarufu bila msingi, umetamania nafsi muhali

Kama nakshi jiweni, elimu uchangani
Sawa nakshi vumbini, elimu ukubwani
Elimu bora duniani, kumcha Mola manani

Mkamate sana elimu, usimwache aende zake
Kwa kila mbinu, mshike asikuponyoke
Ameletewa mwanadamu, kwa ajili ya uzima wake

Tamati Nabii kumsalia, na Ahli zake jamia
Sala na salaam kumfikia, na sahaba zake wasifiwa
Mola atupe afia, atuondoshee kila udhia

IWE MAPENZI KWA WOTE

Mwanzo wa hii nudhumu, jina kuu niliite,
La Mola wetu Qayumu, kinyenyekevu nitete.
Nikuombe ya Rahimu, utubarikie sote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Kwa fututu ya salamu, Tumwa wetu muangate.
Ujumbe wake adhimu, dunia iuzingate.
Dhambi zikose isimu, maovu yatutakate.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Tuongoze wanadamu, adili tuikamate.
Tuepuke udhalimu, katika hali yoyote.
Na utu tuuheshimu, Inda isituokote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Toka kule Kamachumu, mpaka huku Utete
Changamoto zisidumu, kwa vipofu na viwete.
Jamii iwakirimu, Misaada iwakute
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Walinde kwa ukarimu, watoto haki wapate.
Itangazwe ni haramu, kuchapwa hadi watwete.
Na wasichana hirimu, uma usiwakekete.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Wanawake waadhamu, tusiwapigishe kite.
Haki zao tuzikimu, kamwe tusizifumbate.
Tuwape huduma tamu, kizazi chema walete.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Masikini wenye ghamu, kwa shida na hali tete.
Rabi tupe ufahamu, kidugu tuwakumbate.
Tuwatunze kwa nidhamu, kuwahini tusiote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Rushuwa tuone sumu, tuipinge kwa kidete.
Kuisaliti kaumu, hilo mbali litupite.
Tuishi kiisilamu, katika maisha yote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Waongozao kaumu, Manani uwachakate.
Uwajaze utimamu, dola wasiiburute.
Washike vyema hatamu, vileleni watuvute.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Utupe mashamshamu, tusikae bwerekete.
Kwa amali tujihimu, ulofani tusitote.
Maisha yawe karamu, kwa maziwa na mikate.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Awe ni muisilamu, au wa dini yoyote.
Rabana mpe naimu, simwache ajikunyate.
Awapo na hali ngumu, muwezeshe ajipate.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Amani yetu idumu, vurugu zisifukute.
Na siasa chakaramu, za magomvi uzifute.
Vinywani tupe lijamu, matusi yasitokote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Mabeberu wahujumu, nafasi wasiipate.
Mawazo yao hasimu, akili yasituchote.
Tujaalie ugumu, hila zao ziufyate.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Wakituvamia humu, Tusimamie kidete.
Kwa risasi na mabomu, auni tuwakung'ute.
Wabaki kujilaumu, kutuchokoza wajute.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Kungwi natua kalamu, ili wino usikate.
Kwako Rabu Ikiramu, mimi lofa kiokote.
Niliyo yatakalamu, unikubalie yote.
Iwe mapenzi kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Abu Talha, Abdullah H. Mbanga (Kungwi)
99.3 – Radio Ahmadiyya, Mtwara.

Nguvu ya Ukweli

Vijana watatu wa chuo kikuu hawakufanya mtihani kwa sababu hawakusoma na hawakujiandaa.

Wakaja na mpango, wajichafue na oil chafu kisha waende kumwona mwalimu wao wa chuo.

“Mwalimu tunaomba samahani hatukuja kwenye mtihani. Tulikuwa tumehudhuria harusi na wakati tunarudi gari letu lilipata tatizo na hivyo tukachafuka sana kama unavyo tuona”. Mwalimu wa chuo aliwaelewa na akawapa siku tatu wajiandae.

Baada ya siku tatu, walienda kwa Mwalimu wao wa chuo wakiwa wamejiandaa vizuri kwaajili ya mtihani maana walikuwa wamesoma.

Mwalimu wa chuo aliwaweka kwenye madarasa matatu tofauti na kuwapa maswali manne tu kwenye karatasi ya mtihani;

1. Nani alikuwa anaoa au kuolewa? (Alama 25)
2. Sherehe zilifanyika wapi? (Alama 25)
3. Ni wapi hasa gari lilipopata tatizo? (Alama 25)
4. Gari ilipata aina gani ya tatizo?(Alama 25).

Majibu ya kusahihishia: Majibu yenu lazima yafanane.

Hivi tunavyoongea bado wapo kwenye mtihani.

Somo: Ifahamu kweli nayo kweli itakuweka huru.

TAFUTA WANYAMA SITA KATIKA MCHORO

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____



JINSI YA KUPIKA MAANDAZI

MAHITAJI YA MAANDAZI

1. Unga - 5 Vikombe.
2. Tui la Nazi zito vugu vugu - 1 ¼ kikombe.
3. Sukari - 3/4 kikombe cha chai.
4. Samli iliyoyayushwa au mafuta - 3 vijiko vya Supu.
5.Hamirah - 2 Vijiko vya Supu.
6. Hiliki - 1/2 Kijiko cha chai.
7. Mafuta ya kukaangia.



NAMNA YA KUTAYARISHA NA KUPIKA.

1. Ndani ya kibakuli kidogo, mimina hamira na na vijiko viwili vya kulia vya tui. Weka kando mpaka hamira ianze kufura, kama dakika 5-10.

2. Pasha samli moto:
3. Ndani ya bakuli kubwa au sinia, changanya unga, sukari, iliki na samli ikiwa bado moto moto.
4. Mimina hamira ndani ya mchanganyiko wa unga.
5. Changanya na ukande huku ukitumia lile tui la nazi. Tui likipungua unaweza ukaongeza maziwa.
6. Kanda unga mpaka uwe laini.
7. Kata madonge *12 au 15 uyaweke kwenye baraza iliyonyunyiziwa unga na uyafunike ili yapate kufura na yasikauke.

Ukipenda maandazi manene fanya madonge 12.

KUISHI MAISHA YA UNYENYEKEVU NA UMASKINI

Kwa wacha Mungu kulikuwa na sharti hili kwamba waishi Maisha ya Unyenyekevu na Umaskini. Hili ni tawi moja la ucha Mungu ambalo kwalo tunapaswa kukabiliana na hasira isiyojuzu. Kituo cha mwisho na kigumu cha arifu na masiddiki ni kuepukana tu na ghadhabu. Kiburi na majivuno huzalika kutokana na hasira; na vivyo hivyo, wakati mwingine, hasira yenyewe inakuwa matokeo ya Kiburi na majivuno, kwa sababu hasira hutokea wakati Mtu anapojipendelea nafsi yake kuliko mwingine. (Taarifa ya Jalsa Salana, 1897, uk. 49)

Kama nyinyi mnataka Mungu Awe radhi mbinguni, basi mnapaswa muwena umoja kama ndugu wawili wa tumbo moja. Aliyetukuza zaidi miongoni mwenu ni yule anayeyasamehe zaidi makosa ya nduguye, na mwenye bahati mbaya ni yule anayefanya ukaidi na hasamehi, basi huyo hahusiani nami. (Kashtie Nuh (Safina ya Nuhu), Ruhani Khazain, J. 19, uk. 12 -13)

MATUKIO KATIKA PICHA









SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka Uk.12

sababu Qadian huja wageni kila siku, lakini tulipomaliza maombi na kuanza kufanya matembezi ya asubuhi ndani ya eneo hili la makaburi nilimuona Yule kijana kwa ukaribu nikagundua kuwa ni kijana wa Qadian pale pale.

Ukweli ni kwamba kitu ukiwa nacho kila siku wengi tuna tabia ya kukiona cha kawaida na kinapoteza mvuto na msisimko lakini sio kwa watu wa Qadian na watoto wao na vijana, kwani wana yakini ya hali ya juu ya ukweli wa Hazrat Ahmad (as) na hata kidogo hawachukulii mazoea kwa uwepo wao Qadian.

Malezi ya watoto wa Qadian yanafanywa kwa makusudio makubwa na mipango na mikakati inapangwa ya kuwavutia watoto kupitia vitu wanavyovipenda, kupitia michezo, vyakula, mashindano na mazingira rafiki kwa ajili ya watoto kujenga mahusiano mazuri na Jamaat na mafundisho yake.

Maulamaa na Wazee wa Qadian ni omba omba wa dua, kila ukikatiza mtaani au msikitini na kwa uzoefu wangu yeyote atakuita kwa unyenyekevu na kunong'oneza kuwa **'Khakisaar keliye dua ka darkhast he'** yenye maana ya kwamba naomba unikumbuke katika maombi na hio sio mara moja au kutoka kwa mtu mmoja bali ni ada ya watu wote wa Qadian, watakuhimiza kufanya maombi, watakutia nguvu kubaki katika maeneo matakatifu na ufanye maombi zaidi na zaidi.

Mimi shida yangu ilikuwa ni kwa wale wahudumu wanao simamia nyumba ya Masihi aliyeahidiwa (as) na maeneo matakatifu na kuwatembeza watu na kuwaelezea historia za maeneo yale, nilitaka kujua je bado wanashauku kufanya maombi na kusali katika zile sehemu? Kwa yakini nimegundua kuwa kila mfanya kazi ana mda wake maalum wa kuenda na kufanya maombi tena kwa unyenyekevu na vilio zaidi ya sisi tuliotoka mbali, na wanaona haya mno kuonwa wakifanya hivyo. Afisa wa Dar-ul-ziafat siku aliyotupokea na kuongea nasi ofisini mwake, alituambia kama ni kusoma tumeshasoma historia tumepasi Jamia, tulichofuata Qadian ni kufanya maombi katika maeneo matakatifu na kauli hii ilimtoa machozi na kwikwi akiwa mbele yetu.

Watu hulewa fadhili, Na kuziona dhalili

Kauli hii sikweli, Qadian ni mithili

Kuna umaalum mkubwa ndani ya watu wa Qadian hasa mazingira yao na malezi yao kwa ujumla. Siku ya kwanza kufika Qadian nilienda kusali Alfajiri katika Masjid Mubarak, msikiti ambao Hazrat Ahmad (as) aliujenga mkabala na nyumba yake, nilimuona kijana mmoja ambaye alikuwa katika mahangaiko mno kwani mda wa sala ulikuwa umefika na imamu alikuwa hajapita mbele kwa ajili ya sala. Yule kijana alikuwa anaangalia huku na huku na kuonyesha kuwa muda tayari, baada ya mda kupita niligundua kuwa Yule kijana ni bubu hawezi kuongea na uwezo wake wa kiakili hauko sawa, lakini jinsi anavyozingatia muda wa sala utastaajabu, na jinsi anavyosali kwa bashasha itakuathiri. Hazrat khalifat ul Masihi wa nne aliwahi kueleza kuhusu jambo hili kuwa, mazingira ndio jambo muhimu mno katika malezi ya mtu na akasimulia kuwa alikuwepo juha mmoja katika rabwah au Qadian ambaye mwishowe alipotea lakini kabla ya hapo aliaga kuwa anaenda kufanya mahubiri Urusi na akashika njia na hakuonekana tena. Upungufu wa akili sio chanzo cha kutoa lugha chafu na kuwa na tabia mbaya bali mazingira ndio humlisha mtu habari hizo. Qadian nimeshuhudia jambo hili, na kuna kijina mwingine nilikutana naye sokoni kwa kumuangalia tu unamuona huyu ni mpungufu lakini jinsi anavyofanya kazi kwa bashasha na kujituma na mda Fulani nilimuona anaendesha zile baskeli za kubeba watu na muda mwingine nilimuona jikoni akiongeleshana na wabishi na kusaidia kazi. Hivyo basi nimeona kwamba mazingira ni jambo muhimu sana kwa ajili ya malezi ya watoto.

Maulamaa wote wa Qadian wenye majina makubwa wamejitahidi kuwapeleka watoto wao Jamia Ahmadiyya, kana kwamba kila mmoja ana mrithi wake, inavutia mno kuona kuwa Mzee ametumikia Jamaat na mwanaye anatumikia Jamaat au watoto wake wanatumikia Mzee amestaafu. Mimi nilimuuliza Maulana Kaleem-ud-deen ambaye ni Qadhi wa Jamat India, kuwa ameona siri gani mpaka ametoa watoto wake wawili Waqf na wamemaliza Jamia kuwa Mashekh na mtoto wake wa kike amemuozesha kwa kijana ambaye amejitoa Waqf na anaitumikia Jamat hapa hapa Qadian na nilimuweka wazi kuwa jambo hili sio la kawaida katika mazingira yetu.

Sheikh Kaleem ud deen ndiye aliyekuwa msimamizi wa Jalsa Salana 2024 (MC). Siku niliyomuuliza ilikuwa ni zamu yake kutufundisha katika kipindi cha asubuhi na alikuwa anatupa utambulisho wa kitabu kiitwacho **Aina kamalat e Islam**. Mzee huyu alijibu kwa wepesi na umakini sana kuwa yeye huwa alikuwa anawaambia wanawe kuwa mmeniona mimi nimetumikia Jumuiya na hatukuwahi kutembea uchi wala kulala na njaa na wala kudhalilika, hivyo basi inatakiwa mumtumikie Mungu ili maisha yenu yawe na uhakika zaidi, na akaongeza kuwa hili ni jambo la kuwaingizia vichwani mwao na mioyoni mwao tangu wakiwa wadogo. Hawa wenzetu wanaona kutumikia Jumuiya ndio alama ya neema katika familia zao kwani wengi wa Maulamaa ni watoto wa Madarweshi nao wameendelea kuwatoa watoto wao ili kutumikia Jamaat, na hata walinzi wa Qadian wanafanya ulinzi wa maeneo muhimu kwani ni kazi walioirithi nao wanaipenda kwa dhati kabisa.

Ndani yao hawa walinzi na watu wote wa Qadian wanaimani kwa dhabiti kabisa kuwa kazi ya kuilinda Qadian wamechiwa na Khalifa na watapumzika siku Ukhalifa utakaporudi Qadian na wanaamini hiyo siku itafika watakapoikabidhi Qadian katika mikono ya Khalifa. Nyumba ya Huzoor (aba) ipo Qadian ambayo wanafanya kazi ya kuisafisha na kuifunga na kusubiria siku ile.

Nilipata wazo la kupima ufanisi na umakini wa walizi ambao wanafanya ulinzi Qadian hasa wanaolinda mageti ya kuingia msikiti wa Mubarak na Aqsa, nilitaka kuona baada ya kuzoeana na kujuana je wataendelea kunipiga tero? Lakini utaratibu wao uliendelea mpaka mwisho. Baadhi ya walinzi wamepitia jeshini, baada ya kustaafu au kuomba kuacha kazi na kuja kujitolea na kuwa walinzi Qadian, na pia yupo katika ulinzi maalum ambaye aliacha mafunzo ya jeshi na kujiunga na Jamia Ahmadiyya na Kuwa sheikh na yeye ndio msimamizi wa idara ulinzi. Sikuligundua mapema jambo hili kwani huyu jamaa tulikuwa tunacheza naye mpira uwanjani kama mtu wa kawaida.

Tulilokuja kuligundua ni kwamba mji mzima wa Qadian upo chini ya ulinzi wa Waahmadiyya, popote utakapoenda au kutoka nje ya Qadian na harakati zote ndani ya Qadian zinaangaliwa kwa umakini mno. Hata wahindu na watu wengine waishio Qadian hawawezi kufanya chochote kinyume na Waahmadiyya. Tuliona katika suala na usajili wa laini hakuna duka hata moja ambalo walikuwa tayari kutusajilia hata kwa kificho, na hakuna kijana hata mmoja ambaye alikuwa tayari kufanya hivyo hata kwa namna ya kirafiki, kwani inaonekana hata wahindu ambao wanafanya biashara Qadian walishaambiwa hakuna kumsajilia mgeni yeyote laini ya simu mpaka wakati wa Jalsa salana, na kwa ajili ya Jalsa wanasajili laini kwa ajili ya siku kumi tu baada ya hapo laini haitofanya kazi. Jambo la kuzingatia ni kwamba popote tulipokuwa tunatembea tulihisi yupo yeyote ambaye anatufuatilia na kila duka tunaloingia anajua tunachofanya, na umuhimu zaidi ni jinsi gani wanavyofuata maelekezo yaliyotolewa na uongozi hakuna yeyote aliye na shauku ya kuvunja au kutoa mpenyo wa kuvunja maelekezo yaliyotolewa.

Kuna Mzee mmoja alitueleza ya kwamba watu ambao sio waahmadiyya wanawaheshimu waahmadiyya kwa sababu tangu kale walipokuwa na shida yoyote basi walikuja Qadian kwa ajili ya utatuzi wa shida hiyo, kama ni ukame basi walikuja kwa ajili ya dua kwa ajili ya mvua na mvua zilinyesha, kama ni maradhi basi walikuja kwa ajili ya dawa katika Qadian na maradhi walipona, kiasi kwamba vijiji vya jirani vyote kimbilio lilikuwa ni Qadian kwa ajili ya utatuzi wa shida zao zote. Hivyo jambo hili limekaa ndani ya silka zao kuwa Waahmadiyya sio watu wa kawaida tu bali ni watu muhimu mno katika maisha yao.

Qadian na India kwa ujumla nidhamu ya Jamaat imeimarika mno, kiasi kwamba hakuna lolote linalofanywa bila ya ruhusa kutoka idara Fulani ambayo jambo hilo linaratibiwa na kusimamiwa. Miongoni mwetu tulipata shauku ya kutembea kwa miguu kutoka Qadian kwenda Batala kwani Hazrat Ahmad (as) alikuwa akitembea, shauku ilikuwa ni kuonja aliyokuwa akiyapitia na pia kuzuru mji na kupata uzoefu, lakini jinsi ya kupata ruhusa ya kufanya hivyo na mlolongo wake ilibidi shauku hio ikate tu. Nidhamu ya Jamaat katika India imeimarika kiasi kwamba ni kawaida kusomewa majina ya waliotengwa na nidhamu na waliosamehewa

Ukurasa wa 11

SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka uk. 11

na nidhamu mara baada ya sala Fulani, na siri ya uimara huu ni malezi ambayo wanapewa tangu udogo na jinsi wanavyowekwa chini ya uangalizi wa Jamat na kuzoeshwa roho ya utii na kujitolea.

Sadri Khuddam ul Ahmadiyya wa India alitueleza kuwa nidhamu ya Jamaat katika Qadian na India imeimarisha kiasi kwamba kama kukitokea tatizo dogo basi Jamaat nzima inataharuki na kulishughulikia tatizo kwa haraka mno. Alisema kwamba hata wakisikia mtu amempika kofi mkewe basi nidham nzima itataharuki kwani sawa na malezi wanayopewa hilo sio jambo la kawaida kwao.

Eneo hasa linalosisimua hisia uwapo Qadian ni nyumba ya Hazrat Ahmad (as), hisia ambayo nimeipata wakati wa kutembelea Dar ul Masih binafsi na katika ziara maalum ambazo tumeandaliwa na wasimamizi ni hii kwamba, 'ile ngome ya kifalme, na katika historia ya mababu wa Hazrat Ahmad (as) walikuwa ndio watawala na hapa ndipo ilikuwa makao makuu, kwani hata sasa hivi inaonekana kuwa imejengwa katika sehemu iliyoinuka na usanifu wake ni wa hali ya juu mno, na jengo bado ni imara kuishi karne kadhaa zijazo. Ni sehemu ambayo nimehisi kwamba Mwenyezi Mungu ametupa tuonje ladha ya kuzuru ngome ya kifalme huku tukihisi kuwa nasi ni sehemu ya ufalme huu, kwani bila ya kumkubali Masihi aliyeahidiwa (as) ni lini na wapi tungepata fursa ya namna hii.

Mpangilio wa majengo kutoka majengo ya baba zake Hazrat Ahmad (as), yale aliyoyajenga Yeye mwenyewe kwa ajili ya kuishi na yale ya watoto wake. Yale majengo ambayo aliwapa shemeji zake na wakwe zake kwa sehemu ajili ya kujenga na ambayo yaliongezwa na Hazrat Khalifat ul Masih II (ra), ikiwemo Kasr-e-Khilafat na upanuzi na ukarabati wa Masjid Aqswa na Masjid Mubarak yote kwa pamoja ni taswira ya ngome ambayo ufalme wake upo hai ambao ni Ukhalifa na nuru ya Allah imo ndani ya majengo haya. Lakini cha muhimu zaidi ni jinsi gani sehemu za kihistoria zilivyolindwa na kuachwa katika hali yake ya asili kwa hakika unaona dhahiri mpango wa Mungu ndani yake, kwani mara nyingi sehemu za kihistoria hufutwa wakati kukiwa na haja ya upanuzi au ukarabati Fulani sawa na zama.

Na kazi kubwa ambayo imefanyika wakati wa Ukhalifa wa tano haina mfano wake, Dar-ul-Masih ina lifti ya kisasa kabisa na vyoo vya kisasa ndani. Masjid Aqsa imepanualiwa kiasi kwamba umekuwa msikiti wa kisasa ndani ya ngome wenye ghorofa mbili na vifaa vya kisasa kabisa, bustani na uwekwaji wa vigae katika njia na vichochoro vimetia uzuri na ushawishi kwa roho kubakia Qadian,hakika Qadian imenawiri na kushamiri kwa uzuri baada ya ziara ya Hazrat Khalifat ul Masihi V[atba].

Dhana niliyokuwa nayo kichwani kuhusu Qadian na uzuri wake ilikuwa katika mipaka ya picha na makala mbali mbali ambazo nimekuwa nikizifuatilia. Lakini baada ya kufika Qadian uzuri na mvuto wake uliifuta ile picha niliyokuwa nayo kichwani bali uhalisia wa Qadian ni kama ndoto Fulani katika uhalisia wake. Ndoto ya kwenda Qadian nilikuwa nayo tangu mda mrefu, lakini moyoni mwangu nilikuwa nataka ya kwamba baada ya kwenda Qadian basi iwe ndio chanzo cha mabadiliko yangu makubwa ya kimaisha ya utumishi na dunia kwa ujumla. Hivyo nilikuwa nataka nifanye kazi ambayo nitaridhika kwamba nimefanya kitu cha kuonekana na kuniridhisha mwenyewe na hata nikihudhurisha maombi yangu mbele ya Mungu nikiwa Qadian basi ninacho cha kusema kwamba nimefanya kitu fulani. Hivyo miaka yote imepita Mimi nikiwa sina hata shauku ya kutoka nje ya Tanzania kwenda uingereza wala Qadian, nilikuwa natimiza shauku yangu na lengo langu nililojiwekea kwanza, na yeyote aliyekuwa ananiuliza kuhusu mambo haya basi nilimpa jibu hili.

Mchakato wa kwenda Qadian ulianza mwaka 2023 katikati, nilipeleka wazo kwa Amiri na Mbashiri Mkuu kipindi hicho Maulana Tahir Mahmood Chaudhry kwamba tupate nafasi ya kwenda Qadian hata kwa wiki mbili tu ilikupata uzoefu wa hali na mazingira yake. Ushauri wa Maulana Sahib ulikuwa kwamba inabidi tufunge safari katika wakati wa Jalsa Salana na kwa sababu mmoja kati yetu ni Mpakistan, kwa mwaka huu wa 2023 hatutaweza kupata visa yake na kuwahi Jalsa salana kwani mchakato wa visa yake utachukua miezi sita kwa uchache. Hivyo basi inabidi nimkumbushe mwaka unaofuata yaani 2024 mwezi wa tatu, kwa kufanya hivyo muda utapatikana wa kuandika ombi letu kwa Huzoor Anwar (aba) na pia tupate muda wa kushughulikia Visa hasa kwa mwenzetu mwenye passport ya Pakistan.

Mwaka ulivyopinduka na muda ulipowadia wa kumkumbusha Amiri na Mbashiri Mkuu, niliwasiliana na ndugu zangu tutakao safari pamoja juu ya jambo letu na kujaribu kuwauliza ni namna gani kuliendea hili jambo, wote tulikubaliana Mimi ndio nishike dhamana ya kumkumbusha Amiri na Mbashiri mkuu. Jambo la kustaajabisha ni kwamba nilipotuma ujumbe kupitia Email kumkumbusha Amiri na mbashiri mkuu alinijibu kuwa ameshatuma ombi letu kwa Khalifat-ul-Masihi[atba] tayari hivyo ni sisi kufanya maombi na kusubiri.

Jibu lilikuja ya kwamba Huzoor (aba) ameturuhusu na kutuamuru kwenda Qadian kwa miezi miwili kwa ajili ya mafunzo na matembezi. Sheikh Ayyaz Ahmad Dogar alipewa kazi ya kukusanya taarifa zetu na kufanya maombi ya awali ubalozini kwa ajili ya kupata visa, hivyo kuanzia mwezi wa tatu 2024 ilikuwa ni mchakato wa kufanya maombi na wale ambao wahakuwa na hati mpya za kusafiria ilikuwa ndio muda wa kuzifuatilia. Sheikh Ayyaz Ahmad Dogar sahib alipeleka maombi yake mwezi wa tatu kwani mchakato wake ungechukuwa miezi sita kwa upande wetu ilikuwa rahisi sana kwani isingechukua siku moja au mbili kupata visa.

Ulipofika mwezi wa kumi na moja tarehe tano tulichukua visa zetu zenye ruhusa ya utalii kwa miezi mitatu kutoka katika ubalozi wa India mjini Dar es salaam, bila shaka katika mchakato walihitaji kupata taarifa kamili kama waahmadiyya tunaruhusiwa kuingia India ama laa, hivyo ilikuwa rahisi kupata. Kwa upande wangu nilikuwa nimefunga saumu maalum kwa ajili ya hilo ili Allah alete Baraka zake na atie wepesi katika jambo hili. Wahudumu wa ubalozini walivutiwa mno na kujua kwetu lugha ya kiurdu, Bwana Japhet ambaye ni mfanyakazi wa ubalozini pale ambaye ni Mtanzania aliniambia amesoma India kwa miaka mitano lakini hawezi hata kuelewa kiurdu na alishangazwa kuwa tumewezaje kuongea lugha hii. Alikuwa amefurahi na kuvutiwa nasi lakini pongezi hizo hazikutufanya tubweteke katika maombi na kutimiza kila kilichohitajika ili kupata visa zetu. Tulipokuwa Qadian kuna mzee mmoja alitueleza hii siri kwamba, waahmadiyya ni wepesi sana kujifunza hata lugha kwa sababu ya Ukhalifa kwani hata watu wa Qadian ambao sio waahamadiyya hawajui hata kiurdu lakini waahmadiyya wanajua kiurdu na hata kiingereza cha kubabaisha wanakijua na ndio wasomi wa mji.

Baada ya kupata visa zetu ilikuwa ni zamu ya kumuomba Mungu afanye mpango wa kumrahisishia mwenzetu wa nne kupata visa, kwani masheikh waliniambia kuwa huyu hawezi kupata visa na hata Amiri na Mbashiri Mkuu aliniambia kuwa ana wasi wasi mkubwa kuwa India hawatampatia visa kwani haijawahi kutokea hata mara moja kwamba wamempa raia wa Pakistan visa kuingia India hasa kutoka nje ya pakistan. Kwangu mimi ilikuwa kitovu cha maovu yangu na kauli ya kumwambia Mungu sisi ni wanne na wote tunaruhusa ya kwenda Qadian kutoka kwa khalifa wa zama, na nakumbuka nilipata ndoto ambayo ilinionyesha tupo wanne tunaingia uwanja wa ndege kwa ajili ya kusafiri lakini hilo halikunifanya nisiwe na wasiwasi.

Siku moja asubuhi niliingia ofisini nikaamua kumuandikia swali Maulana Ayaz Dogar ujumbe kuwa ndugu zako wahindi wanasemaje kuhusu visa yako?. Akaniambia nakuja Dar es Salaam kwenda ubalozini nikasema Alhamdulillah, mwenzetu alipata visa kwa usumbufu lakini cha ajabu zaidi na muujiza alilipa bei rahisi zaidi kuliko sisi sote.

Tulipofika Qadian hasa wakati wa Jalsa Salana ndio tulijua ni namna gani kuna ugumu mkubwa mtu wa Pakistan kupata visa ya India, waliokuja Jalsa walikuja kwa siku zilizohesabiwa na ulinzi juu, hawaruhusiwi kupiga simu wakiwa India wala kuwasiliana na hawapati laini ya simu ya India.

Safari yetu ilianza Dar es salaam mpaka Muscat Oman, kisha kwenda Delhi, tulipokuwa kwenye sehemu ya mwisho ya ukaguzi Sheikh Tahir alinipa simu yake aliyekuwa hewani alikuwa Amiri na Mbashiri Mkuu, Maulana Sh. Khawaja Muzafar Sahib baada ya salamu tu nikamuwahi Amiri sahib naomba utuombee, akajibu nimewapigia simu hii kwa ajili hiyo, basi tukafanya maombi pale, lakini nilipofika sehemu ya kusubiria nikajua kuwa alimpigia kila mmoja wetu na kuomba naye dua – Alhamdulillah

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE







SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Na.
Sheikh Shaban Othman Shunda



Nilipokuwa Qadian nilipenda kuingia Baitul dua baada ya sala ya adhuhuri kwa ajili ya kufanya maombi kwa sababu zangu binafsi, hasa nilijiona naweza kuwa makini zaidi baada ya kusali rakaa takriban kumi za sunna na faradhi ya adhuhiri hivyo nilipoingia katika kile chumba maalum cha maombi nilijiona mwepesi kuupata umakini wangu na kufanya jambo langu kwa wepesi zaidi. Lakini ninachotaka kueleza ni tukio ambalo nilishuhudia siku moja, nilipoingia nilimkuta mtu mmoja ambaye alikuwa kwenye sujuda, nami nikaanza kusali nafali yangu, lakini jinsi mwenzangu alivyokuwa anasali na kuchemka kwa kilio, nilikuwa najisemea moyoni huyu ni miongoni mwa mashekh wa Ghana ambao wamemaliza Jamia mwaka huu kwani tulikuwa nao kwa ajili ya masomo ya mda mfupi na kuchukua uzoefu jinsi Jamat inavyoendeshwa na utambulisho wa idara zake, na hilo nilikuwa na yakini zaidi kwani kijana aliyekuwa kwenye sujuda alikuwa asili ya rangi nyeusi. Basi niliendelea na sala na maombi yangu nikamaliza nikatoa salamu, nilipomgeukia na kumuangalia angali akiendelea na sala yake nilimuona ni kijana wa kihindi mweusi na umri wake kama amezidi sana ni miaka kumi na mbili au kumi na nne, amewezaje kusali na kuangua kilio namna ile na ni kwanini ameenda kujifungia katika kile chumba kwa yakini ya hali ya juu namna ile kuwa Mwenyezi Mungu anasikia maombi ya aliyedhikika, hayo yalikuwa maswali yangu nilipokuwa natoka katika chumba kile kiitwacho Baitul dua.

Hazrat Ahmad (as) alikijenga chumba hiki mnamo mwaka 1903, maalum kabisa kwa ajili ya kufanyia maombi maalum, naye alikuwa anazungumza na Mwenyezi Mungu katika chumba hiki na ni sehemu muhimu na nyeti mno unapotembelea Qadian na nyumba ya Masihi aliyeahidiwa. Hazrat Ahmad (as) alieleza kuwa ametumwa kwa ajili ya kuwaunganisha watu na Mola wao na hakuna namna wala silaha inayoweza kulitimiza jambo hilo isipokuwa maombi, naye alijenga chumba hiki maalum.

Jibu nililopata baada ya tafakuri ya muda ni kumbukumbu fulani ilinijia, asubuhi ya siku hii nilienda pamoja na wenzangu Bahisht Maqbarah (Makaburi maalum kwa ajili ya waliojiunga na nidham ya wasia kwamba watajitolea sehemu fulani kwa ajili ya kuisaidia kazi ya dini). Na hapa kitu cha kwanza ni kwenda kumuombea Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) katika sehemu ya kaburi lake, pale tulimkuta kijana ambaye alikuwa anafanya maombi na huku akilia na machozi yakitiririka, nikajifariji labda ni mgeni tu ambaye alikuja kutembelea kwa

UK. 10





Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 10,000/=.

Je, Wajua?

Dunia milioni moja zinaweza kujaa ndani ya jua. Jua ni kubwa sana.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com